

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Anuani ya Simu: ELIMU
DAR ES SALAAM
Simu: 2110146-52
Telex 42741 Elimu Tz.
Fax: 2113271
Unapojibu tafadhali taja:



S.L.P 9121
DAR ES SALAAM

14 Februari 2014

Kumb. NaJB.86/287/01/40

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa Temeke,
S.L.P 46343,
DAR ES SALAAM

**YAH: UTARATIBU WA UVAAJI WA VAZI LA 'HIJAB' KATIKA SHULE ZA
MSINGI NA SEKONDARI**

Tafadhali rejea barua yako yenye kumbukumbu namba TMC/DE/P.2/VOL.2/35
ya tarehe 4/2/2014 kuhusu mada tajwa hapo.

Miongozo mbalimbali kuhusu uvaaji 'Hijab' katika shule za msingi, sekondari
na vyo vya Ualimu ilitolewa kwa nyakati mbalimbali na Kamishna wa Elimu.
Kwa bahati mbaya miongozo yote kuanzia ule wa mwaka 1995, 1999 na 2011
haielekezi aina ya Hijab inayotakiwa kuvaliwa shuleni/vyuoni.

Tafsiri na aina ya 'Hijab' inayotakiwa kuvaliwa haikutolewa katika miongozo
hiyo kwa kuamini kuwa vazi la Hijab linaeleweka ni vazi la aina gani.

Hata hivyo kutokana na migongano inayojitokeza katika uvaaji wa vazi hilo,
maelekezo yafuatayo yazingatiwe ili wanafunzi wote wavae vazi linalofanana na
kusiwe na utofauti katika mavazi hayo;

1. Sketi

- iwe ni yenye urefu unaofika katika vifundo vya miguu
- iwe pana na isiwe nyepesi


2. Blauzi (Nusu Kanzu)

- iwe ya mikono mirefu isiyofunika viganja vya mikono
- iwe pana (isibane)
- iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio (isiwe kama gauni)
- isiwe nyepesi

3. kitambaa cha kichwani (ushungi)

- kiwe kipana
- kiwe kirefu kisichofunika viganja vya mikono
- kisifunike uso
- kisiwe chepesi

Vazi lingine la aina yoyote litakalovaliwa kinyume na maelekezo yaliyo hapo juu lisitambulike kuwa ni 'Hijab'


Prof. E.P. Bhalalusesa
KAMISHNA WA ELIMU

✓ Mwenyekiti,
Baraza kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislami Tanzania
DAR ES SALAAM

Mratibu wa Hijab Taifa
DAR ES SALAAM